



Swahili

Kosa la Kutumia Dawa ya Kulevya Ukiwa Unaendesha – Upimaji Zaidi wa Sampuli ya Giligili Yako ya Mdomo

Umepewa Taarifa ya Kosa la kuendesha ukiwa umetumia dawa ya kulevya (**Kosa**). Dhumuni la hati hii ni kukujulisha kuwa sampuli ya giligili yako ya mdomo itatumwa kwenda kwenye maabara iliyoidhinishwa kwa ajili ya upimaji zaidi, na kukupatia taarifa kuhusu jinsi Kosa lako litaakavyoshughulikiwa, kulingana na majibu ya kipimo cha maabara.

Kabla ya kupewa Taarifa ya Kosa, sampuli ya giligili yako ya mdomo ilipimwa na kifaa cha kupima giligili ya mdomo. Majibu ya kipimo hicho yalionyesha sampuli ya giligili yako ya mdomo ilikuwa na dawa ya kulevya isiyohalali.

Kwa uzoefu wa Polisi wa Victoria, vifaa vya kupima giligili ya mdomo vinatoa majibu sahihi kwa vipimo vingi. Ili kuthibitisha majibu yalikuwa sahihi katika kipimo chako, Polisi wa Victoria wataituma sampuli yako ya giligili ya mdomo kwenda kwenye maabara iliyoidhinishwa kwa upimaji zaidi.

Jedwali lifuatalo linaelezea jinsi Kosa lako litakavyoshughulikiwa, **kulingana na majibu ya kipimo cha maabara.**

<p>Ikiwa majibu ya kipimo cha maabara yathibitisha sampuli ya giligili yako ya mdomo ina dawa ya kulevya isiyohalali, Kosa hilo bado linaweza kukutia nguvuni, na wajibu na machaguo yako (kama vile haki yako ya kupinga kosa) zimeelezwa katika Kosa hilo.</p> <p>Ikiwa hili litatokea, hutaarifiwa majibu ya kipimo cha maabara, isipokuwa kama unapinga Kosa hilo.</p>
<p>Ikiwa majibu ya kipimo cha maabara hayathibitisha yawepo dawa ya kulevya isiyohalali katika sampuli ya giligili yako ya mdomo, Kosa hilo litaondolewa, na hakuna adhabu yoyote itakayotolewa kwa Kosa hilo. Ikiwa hii itatokea, Polisi wa Victoria watakujulisha kwa kukuandikia kupitia anwani uliyowapa Polisi wa Victoria. Ikiwa umelipa faini, malipo yako yatarudishiwa.</p>
<p>Ikiwa Polisi wa Victoria hawatapokea majibu ya kipimo cha maabara ndani ya siku 28 baada ya tarehe ya Kosa hilo, Kosa hilo litaondolewa.</p> <p>Ikiwa hili litatokea, Polisi wa Victoria watakujulisha kwa kukuandikia kupitia anwani uliyowapa Polisi wa Victoria. Ikiwa umelipa faini, malipo yako yatarudishiwa.</p> <p>Sampuli ya giligili yako ya mdomo bado itapimwa na maabara iliyoidhinishwa.</p> <p>Ikiwa majibu ya kipimo cha maabara yathibitisha sampuli ya giligili yako ya mdomo ina dawa ya kulevya isiyohalali, utapewa taarifa mpya ya kosa kwa hatia inayodaiwa.</p> <p>Ikiwa majibu ya kipimo cha maabara hayathibitisha yawepo dawa ya kulevya isiyohalali katika sampuli ya giligili yako ya mdomo, hakuna hatua yoyote zaidi itakayochukuliwa.</p>

Unaweza kupinga kosa hilo **ndani ya siku 28** baada ya tarehe ya kosa hilo.

Ikiwa **utakataa** kosa hilo, na majibu ya kipimo cha maabara yakaonyesha sampuli ya giligili yako ya mdomo ina dawa ya kulevya isiyohalali, Polisi wa Victoria watataka suala lako liamuliwe Mahakamani **kulingana na majibu ya kipimo cha maabara.**

Ikiwa **hukukataa** kosa hilo, na katika kipindi cha kukataa majibu ya kipimo cha maabara yanathibitisha sampuli ya giligili yako ya mdomo ina dawa ya kulevya isiyohalali, utakuwa na hatia moja kwa moja kwa kosa hilo, bila kujali kama umelipa faini au la.

Taarifa zaidi juu ya mchakato wa faini inaweza kupatikana katika tovuti ya Fines Victoria kwa <https://online.fines.vic.gov.au/> au kwa kuwapigia simu Fines Victoria kwa namba (03) 9200 8111, kati ya saa 2 asubuhi (8am) hadi saa 12 jioni (6pm), Jumatatu hadi Ijumaa. Wanaopiga simu kutoka Victoria vijijini wanaweza kuwapigia simu Fines Victoria kwa namba 1300 369 819 kwa gharama ya simu ya mahali husika.